BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

# HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA KUSIMAMIA OFISI ZA VIONGOZI WAKUU WA KITAIFA KUHUSU MSWADA WA KUFUTA SHERIA YA BARZA LA WAWAKILISHI (KINGA, UWEZO NA FURSA) NAM. 4 YA 2007 NA KUTUNGA SHERIA MPYA YA BARZA LA WAWAKILISHI (KINGA, UWEZO NA FURSA) KATIKA KUTEKELEZA KAZI NA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO

---

**Mheshimiwa Spika;**

Awali ya yote naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehma, Muumba wa mbingu na ardhi na vyote vilivyomo ndani yake kwa kutujaalia uzima, afya njema na kutuwezesha kufika hapa leo hii tukiwa katika hali ya uzima na amani ambayo imetuwezesha kutekeleza majukumu yetu ipasavyo.

**Mheshimiwa Spika;**

Pia, nimshukuru tena Mwenyezi Mungu kwa kuendelea kuiweka nchi yetu katika hali ya utulivu, na yenye umoja, hali ambayo imeendelea kuipa nafasi Serikali na wananchi wake ambao asilimia kubwa ni wakwezi na wakulima kuweza kutekeleza majukumu yao kwa amani na mshikamano. Aidha, nitumie fursa hii kuiombea Nchi yetu kudumu katika hali ya amani na utulivu kwani bila ya amani hakuna maendeleo yatakayopatikana.

**Mheshimiwa Spika;**

Vile vile, nitumie fursa kwa niaba ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kumpa pole Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Husein Ali Mwinyi kwa msiba mkubwa uliompata wa kuondokewa na kaka yake, hakika ni msiba wetu sote. Tumuombe Allah ampe makaazi mema na awape subra wafiwa wote katika kipindi hichi kigumu.

**Mheshimiwa Spika;**

Aidha, nachukua nafasi hii kukutakia kheri na siha njema kabisa wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ya kusimama mbele ya Baraza lako tukufu kwa ajili kutoa maoni ya Kamati yetu ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kuhusu Mswada wa Kufuta Sheria ya Baraza La Wawakilishi (Kinga, Uwezo Na Fursa) Nam. 4 ya 2007 na Kutunga Sheria mpya ya Baraza la Wawakilishi (Kinga, Uwezo Na Fursa) katika Kutekeleza Kazi na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

**Mheshimiwa Spika;**

Aidha, Kamati pia, inampongeza Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Raisi, Sera, Uratib na Baraza la Wawakilishi – Mhe. Hamza Hassan Juma pamoja na watendaji wake wote wakiongozwa na Katibu Mkuu wake, Naibu Katibu Mkuu pamoja na Katibu wa Baraza la Wawakilishi kwa mashirikiano yao makubwa katika kuhakikisha Mswada huu umekamilika na umekua na tija katika Muhimili huu muhimu sana kwa Nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika;**

Kamati imeelezwa kwamba Mswada huu unakusudia kuondosha kasoro zilizojitokeza katika sheria ya Mwaka 2007 Mswada ambao utaendana na Mazingira ya sasa na baadae kwa Wajumbe mbalimbali wakiwemo wenye mahitaji maalumu kwa kuwatambua wasaidizi wao kisheria, sambamba na kuwawezesha Wajumbe kuitumia Sheria hii katika kutekeleza Majukumu yao

katika Baraza na kazi mbalimbali za Kamati.

**Mheshimiwa Spika;**

Katika kuufanya Mswada huu uwe bora na wenye kupata mafanikio katika utekelezaji wake, Kamati ilipata muda wa kutosha wa kuupitia na kuchambua vifungu mbali mbali ambavyo vimeunda mswada huu ambao lengo lake kuu ni kufanikisha shughuli mbali mbali za wajumbe wa Baraza hili Tukufu.

**Mheshimiwa Spika;**

Kabla ya kueleza baadhi ya marekebisho na mapendekezo kwa ufupi kabisa ambayo Kamati yetu imeyafanya, naomba kuwataarifu Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu ya kwamba, hotuba hii inatoa ufafanuzi tu na msisitizo wa baadhi ya vifungu ambavyo vimependekezwa kufanyiwa marekebisho na Kamati, hivyo maelezo zaidi ya mapendekezo hayo yamo katika marekebisho ya Kamati ambayo Waheshimiwa Wajumbe tayari mmeshapatiwa ili kujisomea kwa ufafanuzi na ufahamu zaidi wa mapendekezo haya.

**Mheshimiwa Spika;**

Katika Kifungu cha 2 cha Mswada huu kamati imependekeza katika tafsiri ya maneno **"Mwenyekiti wa Kamati"** kuongeza maneno mwishoni mwa tasfsiri ya maneno hayo kwa kuongeza maneno yafuatayo ili kuipa ufafanuzi zaidi.

**"na Mjumbe mwengine yeyote atakayechaguliwa na Kamati kuongoza kikao pale ambapo Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti hawapo".**

Sambamba na hilo Kamati imefuta na kuandika upya tafsiri ya maneno **"Afisa wa Polisi",** na kuweka badala yake tafsiri mpya ambayo imefafanuliwa katika Sheria inayohusiana na Jeshi la Polisi ili kuondosha mgongano wa tafsiri hiyo uliojitokeza, na kwasasa inasomeka kama ifuatavyo:

**"Afisa wa Polisi" maana yake ni Mjumbe yeyote wa Jeshi la Polisi kama ilivyotafsiriwa na sheria inayohusiana na Jeshi la Polisi".**

**Mheshimiwa Spika;**

Kamati pia, inapendekeza katika tafsiri ya **"Eneo la Baraza"** kufanyiwa marekebisho kwa kuongezwa maneno **"kupitia Tangazo la Gazeti Rasmi la Serikali"** baina ya maneno **"Spika"** na **"Kuwa"**

ambalo litamuwezesha Spika wa Baraza la Wawakilishi kuweka Mipaka ya Ofisi hiyo kisheria.

**Mheshimiwa Spika;**

Katika tafsiri ya neno **"Mpambe wa Baraza",** Kamati inashauri kufutwa na kuandikwa upya kwa tafsiri ya maneno haya ili kujenga uwelewa mzuri kwa matumizi ya Mswada huu, kama ifuatavyo:

> **"Mtumishi wa Baraza anayeteuliwa na Katibu kwa ajili ya kusimamia itifaki na kudumisha usalama wa Baraza pamoja na kutekeleza shughuli mbali mbali kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu"**.

**Mheshimiwa Spika;**

Katika *Sehemu ya Pili* ya Mswada huu ambayo inaeleza Fursa na Kinga za Wajumbe, Kamati yangu inashauri kukirekebisha kifungu cha 6 Kufuatia ukubwa wa kifungu hicho kwa kukigawanya katika vifungu vidogo vidogo viwili ili kukipa hadhi katika utekelezaji wake, kama ifuatavyo:

**"(1) Bila ya kujali kitu chochote kinachopingana, hakuna wito utakaotolewa na Mahakama au mamlaka yoyote iliyopo Zanzibar au nje ya Zanzibar inayotekeleza mamlaka ya madai au jinai utakaotolewa au kutekelezwa ndani ya eneo la Baraza, kupitia Spika au Afisa wa Baraza, wakati kikao kinaendelea.**

**(2) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (1), Mjumbe yeyote**

**hatakamatwa kwa makosa ya madai wakati Mjumbe yumo ndani ya eneo la Baraza na wakati wa kikao cha Baraza au Kamati kinaendelea isipokuwa kwa ruhusa ya maandishi ya Spika."**

**Mheshimiwa Spika;**

Vile Vile, katika *Sehemu ya Tatu* ya mswada huu ambayo inajumuisha uwezo wa Baraza na Kamati zake kuita mashahidi kwa lengo la kutoa ushahidi mbele ya Baraza au Kamati. Kamati inapendekeza katika Kifungu cha 20(1) kurekebishwa kwa kuingizwa maneno **"maudhui ya nyaraka yoyote iliyowasilishwa mbele ya Baraza au Kamati hiyo kama vile itakavyokuwa au kuhusiana na"** yaliopo baina ya neno **"na"** na **"shauri"**.

**Mheshimiwa Spika;**

Aidha, Kamati inapendekeza katika kifungu cha 30 kurekebishwa kwa kuongeza **aya mpya ya (e)** ambayo itaonesha utambulisho wa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wakiwa katika shughuli za majimbo yao kama wanavyokuwa katika vikao vya Baraza na Shughuli nyengine za Kamati kama ifuatavyo:

**"anamshambulia au anamzuia Mjumbe yeyote wakati anatekeleza shughuli za uwakilishi Jimboni".**

**Mheshimiwa Spika;**

Kwa upande wa *Sehemu ya Masharti ya Jumla ya Mswada huu*, Kamati inashauri kufanyiwa marekebisho kifungu cha 53 ambacho kinampa uwezo Waziri kutunga Kanuni kwa ajili ya utekelezaji bora wa Sheria hii. Aidha, Kamati inashauri kifungu hiki kipewe uwezo wa Mheshimiwa Waziri kushauriana na Spika wa Baraza la Wawakilishi katika kutunga Kanuni zake, kwani Sheria hii itasimamiwa moja kwa moja na Spika wa Baraza. Hivyo, Kamati inapendekeza kuingizwa maneno **"kwa kushauriana na Spika"** baina ya neno **"Waziri"** na **"anaweza"** ili kuweka uwazi na kujenga mantiki sahihi ya

mswada huu.

**Mheshimiwa Spika;**

Kwa kumalizia, naomba kwa heshima kubwa na kwa kuzingatia matakwa ya Wajumbe wa Kamati yangu, naomba sasa uniruhusu niwatambulishe Wajumbe wa Kamati hii kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Machano Othman Said - Mwenyekiti
2. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf - Makamu Mwenyekiti
3. Mhe. Suleiman Makame Ali - Mjumbe
4. Mhe. Zaina Abdalla Salum - Mjumbe
5. Mhe. Salma Mussa Bilal - Mjumbe
6. Mhe. Mohammed Mgaza Jecha - Mjumbe
7. Nd. Ali Alawy Ali - Katibu
8. Nd. Mwanaisha Mohammed Kheir - Katibu
9. Nd. Amina Abeid Hemed - Mkalimani

**Mheshimiwa Spika;**

Mwisho kabisa, naomba kuwashukuru kwa dhati Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kwa kunisikiliza kwa umakini wakati wote ambao naiwasilisha hotuba hii, na pia nizidi kuwashukuru wajumbe wa Kamati yangu kwa mashirikiano yao makubwa waliyonipatia katika kufanikisha kazi zetu.

**Mheshimiwa Spika;**

Aidha, Kamati yangu inawaomba wajumbe wa Baraza hili Tukufu kwamba Mswada huu ulio mbele yetu waujadili na wauchangie ipasavyo na hatimae kuupitisha ili kuwa sheria ambayo itapunguza changamoto zinazowakabili wananchi wetu ambao ndio nguzo pekee ya kulijenga Taifa letu.

**Mheshimiwa Spika,**

Naomba Kuwasilisha.

………………………

(Mhe. Machano Othaman Said)

***Mwenyekiti,***

***Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa.***

BARAZA LA WAWAKILISHI

ZANZIBAR